

Jinsi ya kutumia kipatakilishi cha Chromebook

Hatua ya 1: Uganisha kipatakilishi chako cha Chromebook na pawa ili uchaji kompyuta.



- ✓ Ingiza waya ya chaja kwenye sehemu iliyo upande wa kompyuta.




- ✓ Ingiza upande ule mwingine wa waya kwenye soketi.



Hatua ya 2: Tumia kitufe cha kuwasha ili uwashe Chromebook yako.



- ✓ Chromebook yako ikiwaka, utaona skrini ya kwanza. Itakaa kama picha hii iliyo hapa chini.



Hatua ya 3: Telezesha kidole chako kwenye pedi ya kufuutilia ili usogeze kishale kwenye skrini yako.



Hatua ya 4: Sogeza kishale katika sehemu ya juu ya aikoni ya "Google Chrome" ili ufungua kivinjari cha Intaneti.


- ✓ Aikoni ya chrome imewekwa mviringo hapa chini.



- ✓ Kishale chako kinapogusa sehemu ya juu ya aikoni ya Chrome, itakaa hivi:
- ✓ Bonyeza au gongesha kidole chako kwenye pedi ya kufuatilia ili ufungue Intaneti.



Hatua ya 5: Chrome ikifunguka, andika tovuti unayopewa na shule yako kwenye kivinjari. (Mfano: <https://sites.google.com/dallasisd.org/athomelearningplans/home>)



- ✓ Gonge kitufe cha "enter" kwenye kibodi ili ufikie tovuti.

